**MAFUNDISHO YA BIBILIA**

**KWA WATOTO WA**

**KANISA LA ELOHIM (C. O. G)**

**SIKU YA SABA (7TH DAY)**

**ROBO YA KWANZA**

**2020**

**JANUARI, FEBRUARI, MARCHI**

**KUTUMIWA NA BIBLIA**

**TUMA MAOMBI YOTE KWA**


**3RD ANGEL MESSENGER**

**S. L. P 9774 NAKURU**

**3rdangelmessenger@gmail.com**

**SIMU: +254 721576325 / +254 704590649**

## SOMO LA WATOTO LA JANUARI 4, 2020

## KUZALIWA KWA MASIHI

**Somo kuu: Luka 2**

**Fungu la kukariri : Luka 2:52**

1. Je,manabii walijua Mahali ambapo Masihi angezaliwa? Mika 5:2, Mathayo 2:5
2. Nani alitaka kumuua Masihi? Luka 2:1
3. Nani alikuwa mama yake? Mathayo 1:18
4. Kwa nini Masihi na wazazi wake walienda Misiri? Mathayo 2:13-14
5. Ni lini walirudi kutoka Misiri? Mathayo 2:19-21
6. Ni katika Mji upi waliishi baada ya kutoka Misiri? Mathayo 2:23
7. Katika utotoni wake, je alikuwa ana watii wazazi wake na Elohim? Luka 2:52

## SOMO LA WATOTO LA JANUARI 11,2020

## AMRI

**Somo kuu : Kumbukumbu la torati 5:1-22**

**Fungu la kukariri : Ufunuo 14:12**

1. Nani alipeana amri kumi? Kutoka 20:1-4
2. Nani aliziandika amri kumi? Kutoka 31:18
3. Je,mwokozi wetu alizitupilia mbali amri kumi alipokuja ulimwenguni? Mathayo 5:17-18
4. Tukizitunza amri kumi, je tutapata uzima wa milele? Mathayo 19:16-17
5. Je tumeruhusiwa kuzivunja baadhi ya amri kumi? Yakobo 2:10-11
6. Nani wataruhusiwa katika mji ule mtakatifu? Ufunuo 22:14

7. Nani watakatifu? Ufunuo 14:12

## SOMO LA WATOTO LA JANUARI 18, 2020

## AMRI YA SITA

**Somo kuu : Kutoka 20:1-17**

**Fungu la kukariri : Kutoka 20:13**

1. Amri ya Sita, inatuamuru nini? Kutoka 20:13
2. Nani alituamuru tusiue? Kutoka 20:1-13
3. Masihi alinena vipi kuhusu amri hii? Mathayo 5:21-22
4. Yohana yule mtume alinena vipi kuhusu amri hii? 1 Yohana 3:15
5. Mtu akiwa muuaji, baba yake ni nani? Yohana 8:44
6. Ili tusiwe wauaji, twafaa tufanye nini? Yohana 13:34
7. Je,muuaji ana uzima wa milele ndani yake? 1 Yohana 3:15

## SOMO LA WATOTO LA JANUARI 25, 2020

## MSAMAHA

**Somo kuu: Mathayo 18:21-35**

**Fungu la kukariri: Mathayo 18:21-22**

1. Masihi alipowafunza wanafunzi wake maombi, je aliwafunza kuomba msamaha? Mathayo 6:12
2. Tukisamehea ambao wametukosea, je Elohim atatusamehea? Mathayo 6:14
3. Tusipowasamehe ambao wametukosea, je Elohim atatusamehea? Mathayo 6:15
4. Paulo ametushauri vipi kuhusu Msamaha? Waefeso 4:32

5. Mwandishi wa Zaburi amenena vipi kuhusu Msamaha? Zaburi 130:4,103:3

6. Je Danieli aliomba msamaha kwa niaba ya watu wao? Danieli 9:18-19

7. Ni kwa nani tumepata Msamaha? Wakolosai 1:14,Waefeso 1:7

## SOMO LA WATOTO LA FEBRUARI 1,2020

## IMANI

**Somo kuu : Waebrania 11:1-40**

**Fungu la kukariri : Waebrania 11:6**

1. Imani ni nini? Waebrania 11:1

2. Je, twaweza kumfurahisha Elohim pasipo kuwa na Imani? Waebrania 11:6

3. Ni nini Nabii Habakuki amenena kuhusu Imani? Habakkuki 2:4

4. Ni nani Masihi alimpongeza kwa sababu ya Imani yake kubwa? Mathayo 8:8-10

5. Je, Masihi aliwaamuru watu wawe na Imani kwake Elohim? Marko 11:22

6. Wakati mwanamke mmoja mugonjwa alipomgusa Masihi je Imani yake ilimponya? Luka 8:47-48

7. Je, imani inahitajika ili Mtu awe mtakatifu? Ufunuo 14:12

## SOMO LA WATOTO LA FEBRUARI 8, 2020

## DANIELI

**Somo kuu: Danieli 1**

**Fungu la kukariri : Danieli 1:6**

1. Danieli alikuja vipi katika nchi ya wakalidayo? Danieli 1:1-4.

2. Ni nani wengine walichaguliwa pamoja naye iliwafunzwe lugha ya wakalidayo? Danieli 1:4, 6.

3. Ni majina yapi walipewa na Mkuu wa matowashi? Danieli 1:7.

4. Je, Danieli alipendwa na Elohim zaidi? Danieli 10:11.

5. Nini imesemwa kuhusu Danieli na Nabii Ezekieli? Ezekieli 14:14; 14:20; 28:3.

6. Nini Masihi aliwakumbusha wafuasi wake kuhusu unabii wa Danieli? Mathayo 24:15.

7. Je,Danieli alikuwa akiomba Elohim kila wakati? Danieli 6:10

## SOMO LA WATOTO LA FEBRUARI 15, 2020

## YOHANA MBATIZAJI

**Somo kuu : Mathayo 3:1-17**

**Fungu la kukariri : Mathayo 3:1**

1. Ni Nani walikuwa wazazi wa Yohana Mbatizaji? Luka 1:13

2. Je alikuwa ametabiri kuhusu Masihi? Luka 3:16

3. Je,alimbatiza Masihi? Mathayo 3:13-16

4. Alipokuwa nyikani, alikula nini? Marko 1:6

5. Je,Yohana alifungwa jela? Marko 6:17

6. Nini ilikuwa sababu ya Yohana kufungwa jela? Marko 6:18-19

7. Nini kilifanyika katika jela, je alitoka kutoka jela? Marko 6:21-29

## SOMO LA WATOTO LA FEBRUARI 22,2020

## PETERO YULE MTUME

**Somo kuu : Mathayo 10:1-12**

**Fungu la kukariri : Mathayo 10:2**

1. Nani alikuwa ndugu ya Petero na Mtume wa Masihi pia? Mathayo 4:18

2. Katika wale mitume kumi na wawili wa Masihi nani alijua Masihi ni mwana wa Elohim?Mathayo 16:16

3. Nani alimfunulia Petero ya kwamba, Masihi ni mwana wa Elohim? Mathayo 16:17

4. Jina la Petero lingine lilikuwa lipi? Marko 3:16

5. Je,Petero alikubali watu wamuinamie? Matendo ya Mitume 10:25-26

6. Je, Petero aliwekwa korokoroni kwa sababu ya injili ya Masihi? Matendo ya Mitume 12:1-5

7. Je,Elohim alimtoa kutoka korokoroni? 12:7-11

## SOMO LA WATOTO LA FEBRUARI 29,2020

## YOHANA YULE WA UFUNUO

**Somo kuu : Ufunuo 1:1-20**

**Fungu la kukariri : Ufunuo 1:9**

1. Nani alipewa Ufunuo wa Masihi? Ufunuo 1:1

2. Je,Yohana alikuwa mmoja wa wale mitume kumi na wawili wa Masihi? Mathayo 4:21, 10:2

3. Nani alikuwa baba yake? Mathayo 4:21

4. Baada ya Masihi kupaa mbinguni, je Yohana alikuwa baadhi ya Mitume wale watatu waliokuwa Nguzo ya Kanisa? 2:9

5. Ni ushahidi upi mwingine ambao waonyesha kuwa Ufunuo ulipewa Yohana? Ufunuo 1:14

6. Nani alimuuwa Ndugu yake, Yakobo? Matendo ya Mitume 12:1-2

7. Ni jambo gani lilifanyika wakati Petero na Yohana walipoenda kuomba katika hekalu? Matendo ya Mitume 3:1-11

## SOMO LA WATOTO LA MACHI 7, 2020

## KITABU CHA UFUNUO

**Somo kuu: Ufunuo 1:1-20**

**Fungu la kukariri: Ufunuo 1:1**

1. Nani mwandishi wa kitabu cha Ufunuo? Ufunuo 1:1
2. Kuna baraka ya kusoma Ufunuo? Ufunuo 1:3
3. Nani alionyeshwa Yerusalemu mpya ikishuka kutoka mbinguni? Ufunuo 21:2
4. Je Yohana alionyeshwa mapigo ambayo yataupiga ulimwengu? Ufunuo 9 na 16
5. Ili kuepekuna na mapigo dunia imeshauriwa vipi? Ufunuo 14:9-10 na 18:4
6. Je tumekatazwa kuongeza chochote katika kitabu cha Ufunuo? Ufunuo 22:18
7. Tumenenewa vipi kuhusu malipo katika kitabu cha Ufunuo? Ufunuo 22:12

## SOMO LA WATOTO LA MACHI 14, 2020

## KIFO

**Somo kuu: Mwanzo 3:1-19**

**Fungu la kukariri: Ahibirania 9:27**

1. Nani alikuwa Mtu wa Kwanza kupatana na mauti? Mwanzo 4:8
2. Alipokufa alienda wapi? Mwanzo 4:10-11 patanisha na 3:19
3. Je,kuna kumbukumbu yeyote katika kifo? Zaburi 6:5
4. Ayubu amenena vipi kuhusu kifo? Ayubu 10:22
5. Nini malipo ya dhambi? Warumi 6:23

6. Je,Masihi alishinda kifo? Waebrania 2:14-15

7. Je,kuna kifo cha pili? Ufunuo 21:8

## SOMO LA WATOTO LA MACHI 21, 2020

## KUJA KWA MASIHI MARA YA PILI

**Somo kuu : Matendo ya Mitume 1:1-12**

**Fungu la kukariri : Matendo ya Mitume 1:11**

1. Je, Masihi atarudi tena Mara ya pili? Waebrania 9:28

2. Je,aliahidi kuja tena mara ya pili? Matendo ya Mitume :1:11

3. Ni nini alimwambia mmoja wa mitume wake kuhusu Kuja kwake mara ya pili? Yohana 14:1-3

4. Atakapokuja mara ya pili, je tutatawala naye? Ufunuo 20:4

5. Nabii Zekaria amenena vipi kuhusu kuja mara ya pili kwake Masihi? Zekaria 14:1-9

6. Watu wote wenye watakuwa hai atakaporudi mara ya pili, je wote watamuona? Ufunuo 1:7

7. Nini kitafanyika kwa wale waliokufa wakiwa ndani yake? 1 Wathesalonike 4:16-17

## SOMO LA WATOTO LA MACHI 28, 2020

## UFUFUO

**Somo kuu: Ufunuo 20:1-15**

**Fungu la kukariri: Ufunuo 20:5**

1. Kuna ufufuo mara ngapi? Ufunuo 20:5,20:13

2. Je,kuna ufufuo wa wenye haki? Luka 14:14

3. Je,kutakuwa na ndoa baada ya kufufuka? Luka 20:35-36

4. Je,tumeshauriwa tufunze mafundisho ya ufufuo? Waebrania 6:2

5. Ni kiasi gani cha muda kati ya ufufuo wa Kwanza na wa pili? Ufunuo 20:5

6. Nani watatawala na Masihi? Ufunuo 20:6

7. Je,nabii Isaya alitabiri kuhusu ufufuo? Isaya 26:19